TANGAZO LA SERIKALI Na. 1040 la tarehe 13/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29)*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUBADILI UKUBWA WA ENEO NA JINA LA MSITU WA HIFADHI WA MAZINGIRA ASILIA CHOME KUWA MSITU WA HIFADHI WA MAZINGIRA ASILIA SHENGENA YA MWAKA 2024

KWA KUWA, eneo la Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia la Chome lilitangazwa chini ya Tangazo la Serikali Namba 105 la mwaka 2016 kuwa eneo la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Chome;

NA KWA KUWA, Waziri kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 29 cha Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kubadili ukubwa wa eneo na jina la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Chome kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Shengena; na

NA KWA KUWA, Waziri kwa kuzingatia Sheria ya Misitu ambayo, pamoja na masharti mengine, inamtaka Waziri anapokusudia kubadili ukubwa wa eneo na jina la Msitu wa Taifa wa Hifadhi ya Mazingira Asilia kutoa notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo;

HIVYO BASI, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kubadili Ukubwa wa Eneo na Jina la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Chome kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Shengena ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kubadilishwa

2. Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Chome linapendekezwa kubadilishwa na kuwa kama inavyoainishwa katika Jedwali.

Madhumuni ya mabadiliko

3. Madhumuni ya mabadiliko ya ukubwa wa eneo na jina la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Chome ni -

(a) kujumuisha eneo lote la ardhi ya Hifadhi ya Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Chome baada ya eneo hilo kupimwa upya kwa kutumia njia za upimaji na uchoraji ramani za kisasa kwa ajili ya uhifadhi wa baioanuwai na vyanzo vya maji ili kuendeleza madhumuni ya usimamizi, uhifadhi wa eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo; na

(b) kutumia jina la asili la eneo lililohifadhiwa.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki zinazotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Shengena ambalo linapendekeza kubadilishwa.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza mabadiliko ya eneo na jina la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Chome kuwa Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Shengena, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii, kwa anauani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

JEDWALI


*(Limetengenezwa chini ya aya 2)*

WILAYA YA SAME

MSITU WA HIFADHI WA MAZINGIRA ASILIA SHENGENA

Makadirio ya eneo: Hekta 14,607 au Kilometa za Mraba 146.07 Unakopatikana na Mipaka Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Mazingira Asilia Shengena unaopatikana Wilaya ya Same katika Mkoa wa Kilimanjaro kama lilivyochorwa upya katika Ramani ya Idara ya Upimaji Na. Jb 3172 (Skeli 1:25,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 1040 (Linaendelea)*




Dodoma
11 Novemba, 2024

PINDI H. CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*